Jinsi Ya Kutembea

Na

Ellis P. Forsman

(How To Walk)

Jinsi Ya Kutembea

Na

Ellis P. Forsman

Oktoba 12, 2011

Jinsi Ya Kutembea

Kol. 1:10

Maandiko yanaongelea mienendo ya Wakristo.

- Kol. 1:10, "*Mwenende kama ulivyowajibu wenu kwa Bwana, mkimpendeza kabisa; mkizaaa matunda ya kila kazi njema, na kuzidi katika maarifa ya Mungu.*"
- 1 Thes. 2:12, "*Ili mwenende kama ilivyo wajibu wenu kwa Mungu, mwenye kuwaita ninyi ili mwingie katika ufalme wake na utukufu wake.*"
- Efe. 4:1, "*Kwa hiyo nawasihi mimi niliye mfungwa katika Bwana, <u>mwenende kama inavyoustahili wito wenu mlioitiwa;</u>*"

Kutembea ni muhimu kulingana na mwili wa mtu ulivyo. Madaktari mara nyingi huwaambia wagonjwa watembee kwa sababu ya afya yao.

Inaweza kuwa mbaya kiasi gani kama huwezi kutembea. Alafu, wapo wengi katika dunia hii ambao kwa sababu moja au nyingine hawawezi kutembea au wanaweza kutembea kwa shida kubwa. Mara nyingi wanafikiria ni furaha iliyoje kama wangeweza kutembea.

Biblia inaongelea kuenenda inavyostahili mara tatu.

Hii inamanisha tunatakiwa kujali tunavyotembea – kuenenda inavyostahili. Mienendo yetu ya kila siku inapaswa kuwa bora na Yesu, bora na Mungu, na bora katika huduma yetu kwa Kristo.

Hebu na tujifunze wazo hili la kunenda inavyostahili kidogo kwa karibu.

Tunapaswa kuenenda inavyostahili na Bwana

Kol. 1:10, "*Mwenende kama ulivyowajibu wenu kwa Bwana, mkimpendeza kabisa; mkizaaa matunda ya kila kazi njema, na kuzidi katika maarifa ya Mungu.*"

Hatuwezi kutenganisha mienendo yetu na mapenzi Mungu.

Inamanisha <u>nini</u> kutembea vizuri?

Tunapaswa kuwa wawakilishi bora wa Kristo. Paulo alisema katika Gal. 2:20, "*nimesulubiwa pamoja na Kristo lakini ni hai, wala si mimi tena bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imaani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda akatoa nafsi yake kwa ajili yangu.*"

Kristo alitoa uhai wake kwa ajili yetu nasi tunatoa uhai wetu kwa ajili yake. Kwa vile Kristo anakaa ndani yetu, hatupaswi kufanya chochote cha kuyavunjia heshima makazi yake – hivyo tunapaswa kutembea inavyostahili uwepo wake.

Tuna muwakilisha duniani. Inamanisha kuishi jinsi ambavyo Kristo anaheshimiwa na kutukuzwa ndani yetu.

Kol. 3:17, "*Na kila mfanyalo kwa neno au kwa tendo, fanyeni yote katika jina la Bwana Yesu, mkimshukuru Mungu Baba kwa yeye.*"

Hiii inamanisha, kuheshimu mamlaka yake katika kila jambo; katika tabia zetu binafsi na mienendo; katika maswala yanayofanyika katika mkutano; na katika kila eneo la mawazo na mienendo.

Tunawezaje kutembea vizuri katika Bwana?

Paulo anatoa jibu la neno hili fupi katika Kol. 1:10, "*Mwenende kama ulivyowajibu wenu kwa Bwana, mkimpendeza kabisa; mkizaaa matunda ya kila kazi njema, na kuzidi katika maarifa ya Mungu.*"

"***…mkimpendeza kabisa…***" Kauli hii haipatikani sehemu nyingine yoyote katika Agano Jipya.

Haimanishi (kama watu wengine wanavyofikiria) kuwapendeza wote, lakini inamanisha kumpendeza Bwana katika kila jambo.

Tunapaswa kuwa na mienendo inayompendeza Bwana. tunatembea kumpendeza Bwana kwa sababu tunampenda. 1 Thes. 4:1, "*Iliyobaki ndugu tunakusihini na kuwaonya kwamba mwenende katika Bwana Yesu; kama mlivyopokea kwetu jinsi iwapasavyo kuenenda na kumpendeza Mungu, kama nanyi mnavyoenenda, vivyo hivyo mpate kuzidi sana.*"

Baraka zake ni kwa wale wanaotembea naye na wanampendeza.

"***...mpate kuzaa matunda katika kila kazi njema…***" kuzaa matunda ni ishara ya kuenenda na Bwana.

Wakati mwingine tunakuwa na tafsiri zetu juu ya "*kila kazi njema*" ni nini.

Tunadhani ni mafunzo ya Biblia, kuishi kusafi, kuhudhuria ibada, nk. Lakini ni zaidi ya hayo; pia ni zaidi ya matendo mema yaliyoorodheshwa kaatika Gal. 5:22-23, ambayo tunapaswa kufanya. Gal. 5:22-23, "*Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi; juu ya mambo kama hayo hakuna sheria.*"

Ni huduma yetu ya kila siku kwake na kwamba kila tufanyalo au tunapoingia kwalo ni tendo jemaa, au chema tunachotengeneza katika kila jambo tufanyalo.

"***…kuongezeka katika ujuzi wa Mungu…***" Hii siyo kiakili, au ujuzi wa kidunia, bali ujuzi wa kiroho unaobadilika na kuunda maisha yetu. Yohana 8:32, "*Mtaifahamu kweli nayo kweli itawaweka huru.*"

Kadiri tunavyojifunza katika kusoma Biblia, ndivyo tunavyoweza kumwishia Mungu katika kumpendeza. Zaidi tunavyojua kuhusu

Upendo wa Mungu, huruma, uvumilivu, nk., kadiri tunavyomjua vizuri na ndivyo inaavyokuwa rahisi katika kuenenda kwake.

Sote tunapaswa kutembea katika elimu ambayo sote tunaitwa kwalo

Efe. 4:1, "*Kwa hiyo nawasihi, mimi niliyemfungwa katika Bwana, mwenende kama inavyoustahili wito wenu mlioitiwa.*"

Mwenendo wetu wa kila siku unapaswa kwendana na wito wetu. Tunaitwa wake Kristo, hivyo tunapaswa kuenenda katika yeye.

Yesu alitembeaje?

Maana amesema tujifunze kwake. Mat. 11:29, "*Jitieni nira yangu <u>mjifunze kwangu</u>, kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsini mwenu;*"

Alienenda kwa upole na ukarimu na anatufundisha jinsi ya kuenenda. Mwenendo wetu pia unatakiwa kuwa wa upole na ukarimu, kama jinsi ilivyokuwa kwa Kristo.

Ni lazima tuwe na hisia ya udogo wetu katika mahusiano yetu na Mungu. Yeye ni mkuu zaidi kuliko sisi.

Wale walioongea na Ayubu wanamfahamu Mungu vizuri sana na wakamdhihaki Ayubu kwamba alimtenda Mungu dhambi wakati hakuwahi kutenda dhambi. Mungu anajibu katika Ayubu 38: 1-21… (inaendelea, lakini sote tunasoma tu kupitia ms. 21):

"*Ndipo BWANA akamjibu Ayubu katika upepo wa kisulisuli, na kusema, ni nani huyu atiaye mashauri giza kwa maneno yasiyo na maarifa, kwa maneno yasiyo na maarifa? Basi jifunge viuno kama mwanamume, maana nitakuuliza neno nawe niambie. Ulikuwa wapi nilipoiweka misingi ya nchi? Haya sema kama ukiwa na ufahamu. Ni nani aliyeamrisha vipimo vyake, kama ukijua? Au ni nani aliyenyoosha kamba juu yake? Misingi yake ilikazwa juu ya kitu gani? Au ni nani aliyeiweka jiwe lake la pembeni, hapo nyota za asubuhi zilipoimba pamoja, na wana wote wa Mungu walipopiga kelele kwa furaha? Au ni nani aliyeifunga bahari kwa milango, hapo ilipofurika kana kwamba imetoka tumboni. Nilipoifanya wingu kuwa vazi lake, na giza zito kuwa nguo ya kuifungia, nikaiagiza amri yangu; nikaiwekea makomeo na milango, nikasema utafika mpaka hapa, lakini hutapita, na hapa mawimbi yako yanyetayo, yatazuiliwa? Je umeiamuru asubuhi tangu siku zako zilipoanza? Umeyajulisha mapambazuko mahali pake? Yapate kuishika miisho ya nchi, waovu wakung'utwe wakawe mbali nayo? Ubadilika mfano wa udongo chini ya mhuri, vitu vyote vinatokea kama mavazi. Na waovu nuru yao huzuiliwa isiwafikie, na mkono ulioinuka huvunjika. Je! Umeziingia chemchemi za bahari, au umetembea mahali pa siri pa vilindi? Je! Umefunuliwa malango ya mauti, au umeyaona malango ya kuzimu? Umeyafahamu*

mapana ya dunia? Haya! sema ikiwa unayajua hayo yote. Iko wapi njia ya kuyafikia makao ya nuru? Na giza pia, mahali pake ni wapi? Upate kuipeleka hata mpaka wake, upate kuelewa na mapito ya kuiendea nyumba yake? Hukosi unajua, maana ulizaliwa wakati huo, na hesabu za siku zako ni kubwa!"

Tunahitaji kutembe na upole katika maisha yetu wenyewe. Mungu ni mkuu zaidi kuliko sisi, na tunapaswa kukubali njia zake kuliko zetu. 1 Kor. 10:12, "*Basi adhaniye kuwa amesimama na aangalie asije akaanguka.*"

Yesu alitembea kwa upole. Upole kwa lugha yetu inaweza kutafsiriwa kama "laini", "ukarimu" au "upole".

Siyo "udhaifu", kama jinsi watu wanavyoichukulia siku hizi. Maana hiyo haijatoholewa katika Kiyunani.

Inamchukua mtu mwenye nguvu kuwa mpole wakati wa vitisho au dhihaaka za wengine.

Katika uso wa uelewa huu, tunapaswa kuomba kwamba wengi wetu zaidi tuige tabia hizi tunapoenenda na Mungu.

Yesu alikuwa mvumilivu. Uvumilivu ni upole.

Mungu aalivumilia pomaja na Ibrahimu katika maombi yake kwa ajili ya mji wa Sodoma. Mwa. 18:23-33, "*Ibrahimu akakaribia, aakasema, Je! Utaharibu mwenye haki pamoja na waovu? Huenda wakawapo wenye haki hamsini katika mji, utaharibu, wala hautauacha mji kwa aajili ya hao wenye haki waliomo? Hasha usifanye hivyo, ukamwue mwenye haki pamoja na mwovu, mwenye haki awe kama mwovu. Hasha; mhukumu ulimwengu wote asitende haki? BWANA akasema nikiona katika Sodoma wenye haki hamsini mjini, nitaapaacha mahali pote kwaa ajili yao. Ibrahimu akajibu akasema, basi nimeshika kusema na Bwana, nami ni mavumbi na majivu tu. Huenda wakapunguka watano katika wale hamsini wenye haki, je! Utaharibu mji wote kwa kupungua watano? Akasema sitauharibu, nikiona humo arobaini na watano. Akazidi tena kusema naye, akinena, huenda wakaonekana humo arobaini? Akasema sitafanya kwa ajili ya hao arobaini. Akasema Bwana asiwe na hasira, nami nitasema, huenda wakaonekana huko thelathini? Akasema sitafanya nikiona humo thelathini. Akasema tazama nimeshika kusema na Bwana, huenda wakaonekaana huko ishirini? Akasema sitahajibu kwa ajili ya hao ishirini. Akasema Bwana asiwe na hasira, nami nitasema mara hii tu, huenda wakaonekana huko kumi. Basi BWANA alipokwisha kuzungumza na Ibrahimu, akaenda zake; Ibrahimu naye akarudi mahali pake.*"

Ni uvumilivu kuendelea kusamehe mtu aliyetutenda dhambi. Mat. 18:21-22, "*Kisha Petro akamwendea akamwambia, Bwana ndugu yangu anikose mara ngapi nami nimsamehe? Hata mara saba? Yesu akamwambia sikwambii hata mara saba, bali hata saba mara sabini.*"

Kuvumiliana katika upendo humanisha kuinuliana juu; kuinuana.

Tunapaswa kuvumilia ili kutunza umoja wa Roho katika kifungo cha amani.

- Kuvumilia kunamanisha kujaribu kwelikweli.
- Umoja unamanisha makubaliano.
- Kifungo kinamanisha kile kinachotufunga pamoja.

Kifungo cha amani ni ile inayotokana na upendo, uvumilivu, upole, na kuchukuliana, ambayo hutakiwa katika ukarimu na ukuaji wa Wakristo.

Tunapaswa kutembea katika upya wa uzima

Rum. 6:4, "*Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo nasi tuenende katika upya wa uzima.*"

Tunapofanyika Wakristo, lazima kuwe na hali nzima ya upya katika maisha yetu ambayo huendana na mahusiano yetu na Kristo, na kuishi kwa yeye.

Tumezaliwa mara ya pili kikamilifu. Tazama, yote yamekuwa mapya! Nia njema; mwongozo mpya; kusudi jipya.

Tunapaswa kuenenda kwa upendo

Efe. 5:1-2, "*Hivyo mfuateni Mungu kama watoto wanaopendwa; mkaenende katika upendo; kama Kristo naye alivyowapenda ninyi tena akajitoa kwa ajili yetu, sadaka na dhabihu kwa Mungu, kuwa harufu ya manukato.*"

"Wafuasi wa Mungu" katika tafsiri zingine zinasema "Wanaomfuata Mungu".

Upendo wake umeonyeshwa kwetu kupitia kifo cha mwanaye msalabani.

Tunaonyesha upendo wetu kwake kwa jinsi tunavyofuata upendo wake na kutembea kwayo.

Tunapaswa kuenenda kwwa uaminifu

1 Thes. 4:12, "*Ili mwenende kwa adabu mbele yao walio nje, ...*"

Sisi ni mabalozi wa Kristo ulimwenguni. Hatupaswi kuleta ghadhabu kwa Kristo.

Tunapaswa kuenenda nuruni

1 Yoh. 1:7, "*Bali tukienenda nuruni, kama yeye alivyo katika nuru, twashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu Mwana wake yatusafisha dhaambi yote.*"

Hiyo imanisha nini? Nuru ni neno la Mungu. Tunapotembea, au kuishi katika neno, tunakuwa mbali na dhambi.

Tukifanya hivi, tunakuw na ushirika na kila mmoja, na hiyo inatutia nguvu katika kupigana na dhambi.

Tunapaswa kuwa makini jinsi tunavyoenenda

Efe. 5:15-17, "*Basi angalieni sana jinsi <u>mnavyoenenda</u>; si kama watu wasio na hekima bali kama watu wenye hekima; mkiukomboa wakati kwa maana zama hizi ni za uovu. Kwa sababu hiyo msiwe wajinga, bali mfahamu ni nini yaliyo mapenzi ya Bwana.*"

Kuenenda inamanisha sawasawa, vyema, au makini. Kuikomboa kununua. Wakati ni kipindi cha nafasi.

Wakati ambao haujatumiwa kwa ajili ya Bwana imepotea. Tunapaswa kutembea kwa makini na sawasawa kama Bwana anavyotutaaka kwanzia sasa ili kutengeneza nafasi zile zilizopotea.

Hitimisho

Mtu anwezaje kutembea na Mungu? Mtu ni lazima awe mmoja wa familia yake. Mtu ni lazima afanyike Mkristo. Zifuatazo ni hatua muhimu zinazofanya hilo liwezekane:

- **Imani.** Waeb. 11:6, "Nilipokuwa shuleni (nikiwa na miaka 17), kijana mmoja jirani yangu, umri sawa na wa kwangu alikuwa haamini kuwa Mungu yupo. Kwa vile nilikuwa nimeshabatizwa, nilichukua nafasi ya kuongea naye ana kwa ana kuhusu maandiko. Akaniambia kwamba anaweza kuona kwamba kuishi maisha ya Ukristo ili kuwa ni nzuri. Lakini ili kuwa upande ambao ni salama, labda anaweza kwenda kanisani, na kama akifa na kusimama mbele za Mungu (kama kuna Mungu) siku ya hukumu (kama kuna hukumu), labda kama Mungu akiona kuwa amekwenda kanisani na kuishi maisha mazuri na kwamba Mungu atamruhusu kuingia mbinguni (kama kuna mbingu), na siyo motoni (kama kuna moto). Nikamwambia, "mambo haya hayafanyi kazi kwa njia hiyo. Lazima umwamini yeye kwa moyo wako wote, la sivyo huwezi kumpendeza."
- **Toba.** Matend. 2:38, "*Petro akawambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu katika jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."*

Mdo. 11:18, "..... *Mungu amewapa pia mataifa toba liletalo uzima."* Kama ulikuwa una lala, ukasikia kelele katika chumba kingine, na unafikiria mwenyewe, "kuna mwizi ndani humu!" unachukuwa simu na taratibu unawapigia polisi, ukiwambia kwamba kuna mwizi ndani kwako, na unawapa anwani ya nyumba yako. Kidogo, unawasikia wanafika na kumkamata mwizi. Anapiga kelele, "samahani; samahani!" anaomba msamaha wa nini? Anaomba msamaha kwa sababu amekamatwa; na siyo kwamba ameiba. Katika toba ya kweli mwizi angeomba msamaha

kwamba hataiba tena na anataka kubadilisha maisha yake ili kwamba asiibe tena. Ni badiliko la akili linalo leteleza badiliko la matendo. Hicho ndicho tunachotakiwa kukifanya kabla hatujawa Wakristo.

- **Kukiri.** Warumi 10:9-10*, "Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hatakupata haki, na kwa kinywa hukiri hatakupata wokovu."*

Tunakiri nini? Kwamba tunaamini kwamba Yesu Kristo ni mwana wa Mungu. Kumbuka kwamba katika somo hilo hapo juu imani (kuamini), toba na kukiri ni "**KATIKA**" haki, uzima, au wokovu. "Katika" humaanisha kuelekea kitu fulani; si kwamba mtu tayari ameshapata.

- **Ubatizo.** Ni katika ubatizo ndipo haki inapatikana, uzima, na wokovu vinapatikana. Yesu, mwenyewe, alibatizwa ili kuitimiza haki yote,

"*Lakini Yohana alitakakumzuia, akisema, mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu? Yesu akajibu akamwambia, kubali hivi sasa kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akamkubali. Naye Yesu alipokwisha kubatizwa alipanda kutoka majini, na tazama mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua akija juu yake; na tazama sauti kutoka mbinguni ikisema, Huyu ni Mwanangu, mpendwa mpendwa wangu ninayependezwa naye*." (Math. 3:14-17). Yesu alibatizwa kwa sababu Mungu alisema ni kitu sahihi ya kufanya. Unaona ni jinsi gani ilivyompendeza Mungu wakati Yesu alipobatizwa? Yesu pia alisema "*imekuwa kwetu **sisi** kuitimiza haki yote."* Tunabatizwa kwa sababu inatimiza haki yake yote, siyo kwa sababu ni haki yetu.

Hakika, tusipobatizwa, bado tupo katika dhambi zetu. "*Petro akawambia, tubuni makabatizwe kila mmoja wenu kwa jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."* (Matend. 2:38). Petro, ulisema ubatizo ni kwa ajili ya nini? *"Kwa ajili ya ondoleo la dhambi."* Kwa nini mtu mwingine anaacha hatua hii muhimu inayoondoa dhambi zetu?

Yesu aliamuru kwamba ili kuufikia wokovu ni lazima tubatizwe. *"Akawaambia, enendeni ulimwenguni mwote mkahubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye **na** kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa."* (Marko 16:15-16).

Anania alimwambia Sauli (kabla hajaitwa Paulo) kitu kama hiki, "*Sasa unakawilia nini? Simama, ukabatizwe uoshwe dhambi zako, ukiliitia jina la Bwana."* (Matend. 22:16).

Ubatizo ni agizo lililotolewa na Mungu.

Ubatizo unaitwa maziko. "*Hivyo mnazikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake: kama vile Kristo alivyofufuka katika wafu kwa utukufu wa Baba, hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima."* (Waru. 6:4). Utu wetu wa kale ni lazima ufe. *"Hamfahamu ya kuwa sisi sote*

tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlivyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaungana kwa mfano wa kufufuka kwake; mkijua neno hili, ya kuwa utu wetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena." (Rum. 6:3-6).

Ubatizo ni ramani ya Mungu kwa kutumia damu ya Kristo katika maisha yetu kwa njia ya ubatizo. Tunakuwa huru kutoka katika dhambi zetu za zamani pale tu tunapobatizwa.

Hii haimaanishi "kunyunyiza. Andiko hapo juu inasema ubatizo ni maziko. Hatuendi makaburini na kuchukua udongo kidogo na kuweka juu ya mwili wa marehemu.

Kama hujafanyika mshiriki wa kanisa la Kristo, kwa nini usizingatie leo?